



THE CATHOLIC UNIVERSITY OF EASTERN AFRICA

A. M. E. C. E. A

**P.O. Box 62157
00200 - City Square
Nairobi - Kenya
Tel: 254-20-890095
Fax: 254-20-891261
E-mail: academics@cuea.edu**

This Degree Programme Was
approved by the Commission for
University Education on:

14 AUG 2014

[Handwritten Signature]

Authorized Signature

**SHAHADA YA UZAMILI KATIKA KISWAHILI NA
MAWASILIANO**

**Imewasilishwa Kwa Halmashauri Ya Elimu Ya Vyuo Vikuu,
NAIROBI**

Februari, 2014



14/5401

2.0 Shahada ya Uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano

2.1 Anwani ya shahada iliyopendekezwa

Anwani ya shahada hii ni Shahada ya Uzamili katika Kiswahili na Mawasiliano.

2.2 Falsafa ya Programu Hii

Programu hii inanuiwa kuwahitimisha wasomi wenye maarifa ya kiwango cha juu katika Isimu, Fasihi na Mawasiliano na ambao wana maadili ya kuitumikia jamii kwa haki na ukweli katika misingi ya maadili ya kikristo.

2.3 Umuhimu wa Programu Hii

Uanzishaji wa programu hii unalenga kukidhi mahitaji makubwa ya wataalamu waliobobea katika isimu, fasihi, pamoja na mawasiliano katika eneo la Mashariki mwa Afrika. Uchunguzi uliotangulia maandalizi ya kozi hii ulibainisha kuwepo kwa uhaba mkubwa wa wataalamu katika nyanja hizi.

2.4 Madhumuni ya Jumla

Programu ya M.A. (Kiswahili na Mawasiliano) inalenga kutoa fursa kwa washiriki kupata kiwango cha juu cha utaalumu katika uchambuzi, uchanganuzi na uhakiki wa masuala mbalimbali yanayohusiana na usomi wa lugha, isimu, fasihi ya Kiswahili na Mawasiliano. Programu hii inawaandaa washiriki kuweza kukabiliana na changamoto zilizoko kwenye sekta mbalimbali zinazoshughulika na masuala ya lugha, isimu, fasihi na mawasiliano, ikiwa ni pamoja na ufundishaji katika vyuo vikuu, katika misingi ya ukweli na uadilifu.

CUEA ni asasi ya Kikatoliki ya masomo ya juu iliyoasisiwa na kuendeshwa kwa msaada wa Jumuiya Wanachama wa Muungano wa Maaskofu wa Afrika Mashariki (AMECEA). Kwa kariha ya maneno ya Yesu Kristo, "Wakifu katika Ukweli (Yh 17:17)", inalenga kukuza utafiti wa kisayansi, ufundishaji bora na hudumu stahiki ya jamii kwa kusudi la kuimarisha maisha ya Ukristo.

Katika misingi ya neno la Mungu, desturi dumu na mafundisho ya kanisa yaliyo bia na ya kimaeneo; inatoa programu ambazo zimeundwa kuwaandaa watoa huduma wanaostahili kwa kanisa na jamii.

Vilevile, inalenga kukuza mahusiano na ushirikiano na vyuo vingine vikuu kwa lengo la kujenga jamii bora ya wanadamu.

2.5 Malengo Mahsusuni

Programu ya M.A. katika Kiswahili na Mawasiliano inalenga kuwawezesha wanafunzi:

- i) Kutumia maarifa ya kozi hii katika kuyachanganua na kuyawasilisha masuala yanayohusiana na Isimu ya Kiswahili, Fasihi ya Kiswahili na Mawasiliano katika Kiswahili; kwa misingi ya ukweli na uadilifu.
- ii) Kutekeleza utafiti wa kisayansi juu ya mada mbalimbali za kiisimu, kifasihi na kimawasiliano kwa kutumia mbinu za kisayansi ili kuibua majibu na kauli zenye manufaa kwa jamii kwa jumla.

- iii) Kuitumia lugha ya Kiswahili kama ala mahsusi ya mawasiliano.
- iv) Kuweza kuhusisha nadharia za kiisimu na za kifasihi katika kuifundisha lugha hii katika viwango vya juu.
- v) Kutekeleza kikamilifu shughuli za sekta mbalimbali zinazohusiana na lugha ya Kiswahili na mawasiliano; na hivyo, kuchangia katika maendeleo ya taifa na ulimwengu kwa jumla.

2.6 Mtindo wa Ufundishaji

Ufundishaji utafanywa kwa njia ya wahadhiri kukutana ana kwa ana na wanafunzi chuoni. Aidha, wanafunzi watahusishwa katika majadiliano, mawasilisho ya darasani pamoja na utafiti wa maswala mbalimbali.

2.7 Mahitaji ya Shahada

2.7.1 Masharti ya Usajili

- a) Masharti yanayohusu shahada za uzamili katika chuo kikuu yatatumika.
- b) Masharti yanayohusu shahada za uzamili (MA) katika Kitivo cha Sanaa na Sayansi za kijamii yatatumika.
- c) Idara itasajili:
 - i) Walio na shahada ya kwanza ya B.A. au B.Ed (Arts) katika Kiswahili, daraja ya "Lower Second with Honours" kutoka katika Chuo Kikuu Katoliki cha Afrika Mashariki wataruhusiwa kujiunga na programu ya M.A. (Kiswahili na Mawasiliano).
 - ii) Walio na shahada ya kwanza ya B.A. au B.Ed (Arts) katika Kiswahili, daraja ya "Lower Second with Honours" kutoka katika vyuo vikuu vingine vinavyotambuliwa na Chuo Kikuu Katoliki cha Afrika Mashariki pamoja na Elimu ya Juu nchini Kenya wataruhusiwa kujiunga na programu ya M.A. (Kiswahili na Mawasiliano).

2.7.2 Mahitaji ya Kozi

Kwa jumla kozi hii itamhitaji mwanafunzi ahudhurie madarasa, kufanya utafiti na kuwasilisha makala darasani, kufanya utafiti, kuandaa na kukamilisha tasnifu ya utafiti huo.